# Ofisi ya Rais
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

MKOA WA ARUSHA
Barua zote ziandikwe kwa Mkuu wa Shule
Simu Na. +255 752 954 965

**Email;irkisongoss@ gmail.com**

IRKISONGO SECONDARY,
S.L.P. 43,
MONDULI ,

IRKISONGO SECONDARY SCHOOL
EDUCATION FOR LIBERATION

---

**Kumb.Na. MOND/IRK/SS/GF.2024** **Tarehe_________________**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IRKISONGO HALMASHAURI YA MONDULI, MKOA WA ARUSHA.**

**Ndugu mzazi/mlezi,** Uongozi wa Shule ya Sekondari Irkisongo unayo furaha kukuarifu kuwa mwanao ___________________________________________________________________________ amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Irkisongo sekondari mwaka 2024. Shule ya Irkisongo sekondari ipo umbali wa kilometa 45 kutoka Arusha mjini na usafiri wa kutoka Arusha mjini unapatikana kituo cha mabasi ya stendi ndogo kwa nauli ya sh. 2,000/= hadi Monduli mjini.

Shule ipo Monduli mjini Kaskazini mwa kituo cha mabasi Monduli hatua 300 kutoka kituoni. Shule yetu ni ya wasichana tu kidato cha kwanza hadi cha sita.

Shule itafunguliwa tarehe 08/01/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 08/01/2024.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**1. VIFAA VYA DARASANI**

i. Madaftari makubwa **12 "COUNTER BOOK"QUIRE 3**
ii. Mkebe "Mathematical Set"
iii. Kamusi ya Kiingereza kwa kingereza
**iv.** Kalamu za kutosha (bluu na nyeusi), rula na penseli
**v.** Karatasi za kufanyia mazoezi yake ya jioni **(Rim moja)** aina ya **"PAPER LINE** au **TRION"**.
**vi.** Aje na ufagio wa kawaida (chelewa) kwa ajili ya usafi.

**2. SARE ZA SHULE**

- **i.** Sketi mbili, rangi damu ya mzee marinda ndefu mpaka kwenye kisigino.
- **ii.** Shati mbili nyeupe Tetron mikono mirefu isiyobana mwili.
- **iii.** Viatu vyeusi vya ngozi na sio vya ghorofa, vya kufunga kamba.
- **iv.** Sweta rangi damu ya mzee shingo "V" lisilo la mtumba lenye mistari meupe shingoni na mkononi.
- **v.** Soksi ndefu nyeupe jozi mbili zifike kwenye magoti (Stocking)
- **vi.** Tai nyeupe yenye miraba ya damu ya mzee.
- **vii.** Picha paspoti (PPS) 2 za baba na mama au mlezi.
- **viii.** Hijabu mbili nyeupe zinazofika mabegani kwa waislamu isiyo na mapambo yoyote (Plane white).

**3. SARE ZA KUVALIWA BAADA YA MASOMO**

- **i.** Gauni ndefu rangi DAMU YA MZEE la kushona (SOLO) kitambaa cha tetron nzito. *(kitambaa kama cha sketi)*
- **ii.** Track suit ya kuvaliwa usiku (rangi ya DAMU YA MZEE yenye mistari myeupe pembeni)
- **iii.** T – Shirt ya rangi **DAMU YA MZEE** nzito yenye kola isiyo na maandishi wala picha
- **iv.** Raba kwa ajili ya michezo
- **v.** Bukta ya rangi ya **DAMU YA MZEE** kwa ajili ya michezo.
- **vi.** Mabuti ya kuvaa wakati wa mvua (rain boot)
- **vii.** Mwamvuli mmoja

**4. VIFAA VYA HOSTELI**

- i. Godoro moja jipya la kitambaa urefu futi 6 na upana futi mbili na nusu (6 kwa $2^{1}/_{2}$)
- ii. Shuka mbili za rangi DAMU YA MZEE
- iii. Blanketi moja zito.
- iv. Sanduku la bati lenye kufuli imara (tranker)
- v. Chandarua cheupe cha kuzuia mbu
- vi. Taulo au Doti moja ya kitenge cha kujifunga wakati wa kwenda kuoga tu pamoja na ndala jozi moja **(haruhusiwi kuvaa kitenge wala ndala nje ya bweni)**
- vii. Taulo za kike (Pedi) za kutumia kila mwezi na nguo za ndani za kutosha
- viii. Dawa ya meno, mswaki, mafuta ya kujipaka na sabuni( **Hairuhusiwi kutumia vipodozi vya aina yoyote)**
- ix. Ndoo ndogo mbili za lita kumi kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa na kuogea

x. Tochi ya betri au taa ya kutumia mwanga wa jua. (**hairuhusiwi kutumia taa inayotumia umeme, mafuta ya taa au mshumaa)**

xi. Fagio mbili (2) za chelewa

**5. VYOMBO VYA CHAKULA.**

**i.** Sahani ya bati (aluminium) yenye sehemu ya mboga ugali na matunda.

**ii.** Kikombe kimoja cha bati (aluminium) nusu lita

**iii.** Kijiko (**vyombo vya plastiki haviruhusiwi kabisa)**

**A. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekibishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini yaani Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendashaji wa Elimu.

**MUHIMU.**

- Kama mwanafunzi ana bima ya afya aje nayo kwa ajili ya matibabu. Shule ina zahanati inayotoa huduma ya kwanza.Aidha matibabu yanapatikana Hospitali ya Wilaya kwa gharama za mzazi au mlezi hali ikiwa mbaya. Shule haitoi chakula maalum kwa wanafunzi wenye matatizo ya kiafya kwani chakula cha shule ni kizuri.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani
- Mwanafunzi haruhusiwi kwenda hosteli bila kukamilisha usajili
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula chochote shuleni
- Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa kuripoti kwa tarehe iliyopangwa.
- Mwanafunzi haruhusiwi kupaka kucha rangi, kupaka lipstick,au kupaka wanja
- Mwanafunzi aje amenyoa nywele kawaida na sio mitindo yoyote.
- **Kuweka alamza kwenye kila kitu cha mwanafunzi kuepuka usumbufu. Kwenye sare zote majina ya mwanafunzi yaandikwe kwa mashine kwenye belt au kwenye kola**

**B. FOMU F1, na F2,**

**FOMU F2** ijazwe na Daktari aliyeidhinishwa, fomu F1 ijazwe na mwanafunzi mwenyewe na mzazi au mlezi au taasisi husika. Fomu zote 2 zirudishwe shuleni mwanafunzi anaporipoti.

**“SIMU YA MKONONI HAZIRUHUSIWI KABISA KWA MWANAFUNZI NA ENDAPO ATAKUTWA NAYO MWANAFUNZI HUYO ATASIMAMISHWA MASOMO.**

**“**ELIMU NI UKOMBOZI**”**

KARIBU SANA IRKISONGO ...............................................

**NYANYAMA B. CHIREMEJI**

**MKUU WA SHULE**

**SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI NA MWANAFUNZI** **F1**

1. **AHADI YA MZAZI/MLEZI KUHUSU MALEZI YA MTOTO.**

Mimi ........................................................... ambaye ni mzazi/mlezi wa manafunzi ............................ ninaahidi kumhudumia mwanangu na kumpatia mahitaji yake kwa wakati na kushirikiana na shule kumlea mtoto huyu. Aidha ninaahidi kwamba nitahakikisha mwanangu atasoma na kumaliza shule na hivyo sitakubaliana na utoro wa aina yeyote.

Nitashirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha mwanangu wa kike hatapata ujauzito wala sitamuoza au kupokea mahari wakati wote wa masomo yake. Endapo nitakiuka ahadi hii hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

Saini ya mzazi/mlezi................................tarehe...........................simu...........................................

**2. MZAZI/MLEZI/ TAASISI ITAYOGHARAMIA MAHITAJI YA SHULE:**

(i) Jina …………………………………………………………………………………………………….

(ii) Kazi yake ni ………………………………………………………………………………………….

(iii)Anuani ya mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………………

(iv) Namba yake ya simu……………………………………………………………………………………

(v) Uhusiano wake…………………………………………………..Mf. Baba, Mama, Dada, Mjomba au mfadhili

3. **UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI**:

Mimi ………………………………….…...... nakubali kujiunga na shule ya **IRKISONGO SEKONDARI** na kuthibitisha kuwa, nitafuata sheria na taratibu zote za shule hii ili nitimize lengo la kuja shuleni kwa manufaa yangu binafsi, familia na Taifa kwa ujumla. Endapo nitakwenda kinyume na sheria/kanuni na taratibu za shule nitakubali hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria zichukuliwe dhidi yangu.

**Sahihi ya mwanafunzi ………….......................……………..tarehe……..........................**

## 4. NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

Mimi mzazi/mlezi nadhibitisha kuwa waliojiandikisha hapo chini ni ndugu zangu wa karibu ambao wanaweza kuruhusiwa kumtembelea mtoto wangu na pia shule inaweza kufanya mawasiliano nao kwa masuala yanayomuhusu mwanafunzi huyu.

| S/N | MAJINA MATATU | UHUSIANO NA MTOTO | PICHA YAKE (PASSPORT SIZE) | SIMU YA MKONONI | SAINI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |

**NB: hataruhusiwa mtu ambaye si mhusika na hajaorodheshwa kwenye fomu kuja kwa masuala yanayo muhusu mwanafunzi shuleni.**

**F2**

**PRESIDENT`S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**IRKISONGO SECONDARY SCHOOL**

**<u>MEDICAL EXAMINATION</u>**

To THE MEDICAL OFFICER (GOVERNMENT HOSPITAL)

...................................................................

....................................................

Please examine the above named student and arrange for any necessary treatment for a student if need be.

HEADMISTRESS
IRKISONGO
SECONDARY SCHOOL

**THE HEADMISTRESS.**

Student's full name:……………………………………Age:-……………......Year...........

REMARKS

SKIN...................................................................................................................................

EYES...................................................................................................................................

EARS...................................................................................................................................

TEETH.................................................................................................................................

B/S TEST (CHRONIC)......................................................................................................

PRESURE..........................................................................................................................

ABDOMEN.......................................................................................................................

CHEST...............................................................................................................................

STOMACH.........................................................................................................................

URINE................................................................................................................................

HB.HAEMOGLOBIN........................................................................................................

T.B TEST:-……………………………………………………………..........................................

VDRL..................................................................................................................................

HIV TEST...........................................................................................................................

UPT TEST...........................................................................................................................

STOOL................................................................................................................................

ULCERS..............................................................................................................................

DIABETIC...........................................................................................................................

ASTHMATIC......................................................................................................................

Doctors Name.......................................... Signature:………………………

Designation …………………………............ Station …………………………

# SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE KWA WANAFUNZI

## 1. Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria, Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamira ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo yanayofafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 1.1 Sheria na kanuni za shule

**(a)** Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

**(b)** Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.

**(c)** Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation)

**(d)** Kuwahi katika kila shughuli za Shule utakazopewa

**(e)** Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.

**(f)** Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule

**(g)** Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

**(h)** Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

**(i)** Kutunza mali za shule

**(j)** Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari na;

**(k)** Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kushawishiwa na mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

## MUHIMU;

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa shule. (Msiba au Ugonjwa)

**1.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na;**

- **a.** Wizi
- **b.** Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
- **c.** Kugoma na kuhamasisha mgomo.
- **d.** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
- **e.** Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
- **f.** Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
- **g.** Kufuga ndevu.
- **h.** Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
- **i.** Uvutaji wa sigara.
- **j.** Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa.
- **k.** Kupata ujauzito au kutoa mimba.
- **l.** Kusababisha mimba.
- **m.** Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- **n.** Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
- **o.** Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- **p.** Kudharau bendera ya Taifa.
- **q.** Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu na;
- **r.** Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**3. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa shule**

**Jina la Mkuu wa shule: <u>NYANYAMA BWIRE CHIREMEJI</u>**

**Mhuri wa Mkuu wa shule** HEADMISTRESS IRKISONGO SECONDARY SCHOOL

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

*TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO;*

- **Mkuu wa shule: 0752 954 965**
- **Makamu mkuu wa shule: 0629 926 755**
- **Mwandamizi Taaluma: 0788 526 398**
- **Mwandamizi malezi: 0758 463 574**